**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA**

**MTIHANI WA UALIMU DARAJA LA A**

**621** **KISWAHILI**

**Muda: Saa 3.** **Jumatatu, 09 Mei 2011 mchana**

---

**MAELEKEZO.**

1. Karatasi hii ina sehemu **A**, **B** na **C.**

2. Jibu maswali **yote** katika sehemu **A** na maswali **mawili (2)** kutoka kila sehemu **B** and **C**.

3. Sehemu **A** ina alama **arobaini (40)** na sehemu **B** na **C** zina alama **thelathini (30)** kila moja.

4. Vifaa vya mawasiliano na vitu vyote visivyoruhusiwa **havitakiwi** ndani ya chumba cha mtihani.

5. Andika **namba yako ya mtihani** katika kila ukurasa wa kijitabu chako cha kujibia.

maktaba.tetea.org
TETEA


Find this and other free resources at: https://maktaba.tetea.org

## SEHEMU A (Alama 40)

Jibu maswali **yote** katika sehemu hii

1. Toa hoja nne za kuthibitisha nafasi ya Kiswahili katika elimu ya juu.

2. Eleza tofauti nne kati ya methali na misemo.

3. Eleza faida nne za kutumia nyimbo shuleni.

4. Toa hoja nne za umuhimu wa Kiswahili kama chombo cha kufundishia.

5. Eleza mambo manne ya kuzingatia katika maandalizi ya hotuba ya Kiswahili.

6. Taja vigezo vinne vya kutunga malengo mahsusi ya somo.

7. Eleza mchango wa kazi za fasihi simulizi katika kudumisha mshikamano wa kijamii.

8. Toa hoja nne za kuthibitisha nafasi ya Kiswahili katika nyanja za kidiplomasia.

9. Eleza sifa nne za maandiko bora ya vitabu vya ziada.

10. Toa hoja nne zinazoonyesha faida za wanafunzi kushiriki katika mijadala ya Kiswahili.

## SEHEMU B (Alama 30)

Jibu maswali **mawili (2)** kutoka sehemu hii.

11. Eleza mchango wa vitendawili katika kuimarisha ufasaha wa wanafunzi.

12. Toa hoja tano za umuhimu wa kazi za ushairi katika kufundisha lugha.

13. Jadili nafasi ya nyimbo katika kukuza mshikamano wa kitaifa.

14. Eleza hatua nne zinazofuata mwalimu anapopanga ratiba ya somo la Kiswahili.

## SEHEMU C (Alama 30)

Jibu maswali **mawili (2)** kutoka sehemu hii.

15. Eleza sifa tano za mbinu bora za ufundishaji wa Kiswahili.

16. Toa faida tano za mitihani midogo midogo kwa wanafunzi.


Find this and other free resources at: https://maktaba.tetea.org

17. Eleza mbinu tano za kufundisha sarufi ili kuwahimiza wanafunzi kushiriki darasani.

18. Jadili mambo matano yanayomsaidia mwanafunzi kukuza stadi za kuandika kwa ufasaha.


Find this and other free resources at: https://maktaba.tetea.org